JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# TOLEO MAALUM LA MWANANCHI




## Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka wa Fedha 2023/24

Machi 2025

# YALIYOMO

YALIYOMO ii
UJUMBE WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI 1
MUHTASARI 3
SURA YA KWANZA 5
UTANGULIZI 5
SURA YA PILI 7
HATI ZA UKAGUZI WA HESABU NA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI 7
SURA YA TATU 12
MASUALA YA JUMLA NA HOJA MTAMBUKA ZA UKAGUZI 12
SURA YA NNE 15
UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU 15
SURA YA TANO 20
UKAGUZI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA 20
SURA YA SITA 28
UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA 28
SURA YA SABA 40
UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO 40
SURA YA NANE 45
UKAGUZI WA UFANISI 45
SURA YA TISA 51
UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA 51

## SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI



**Ndugu Mwananchi,**

Ninayo furaha kukuletea Ripoti yangu ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024 kupitia Toleo Maalum la Mwananchi. Toleo hili linalotoa muhtasari wa Ukaguzi nilioufanya katika Serikali Kuu, Idara na Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Miradi ya Maendeleo pamoja na Kaguzi za Ufanisi.

Kupitia toleo hili ambalo hutolewa kila mwaka na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), tunatekeleza matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria husika za Ukaguzi wa Umma, pamoja na viwango vya kimataifa vya INTOSAI (International Organization of Supreme Audit Institutions). Hasa tunazingatia Kanuni ya INTOSAI P-12, inayosisitiza uwajibikaji kwa wananchi na uwazi katika utendaji wa Taasisi Kuu za Ukaguzi.

Lengo la toleo hili ni kukushirikisha wewe, Mwananchi, katika mchakato wa Ukaguzi kwa kukupatia taarifa juu ya matokeo ya Ukaguzi yaliyofanywa na Ofisi yangu. Tunaamini kuwa kwa kutumia lugha rahisi na ya wazi, tunachangia kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za Umma.

Katika toleo hili, pamoja na kaguzi nyingine za kifedha na za ufanisi, pia utapata matokeo ya kaguzi za mifumo ya TEHAMA, ambazo ni muhimu katika kuhakikisha matumizi bora ya mifumo ya kidijitali katika taasisi za Umma.

**Wito kwa Wananchi**

Ninawaomba wananchi wote kutumia taarifa zilizomo katika ripoti hii kushiriki kikamilifu katika usimamizi wa rasilimali za Umma. Ushiriki wenu unachangia kwa kiasi kikubwa katika kuhakikisha kuwa fedha za Umma zinatumika kwa ufanisi, uadilifu na kwa malengo yaliyokusudiwa.

Tafadhali toa maoni na mapendekezo yako kuhusu jinsi ya kuboresha utendaji wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kwa kushirikiana pamoja, tunaweza kujenga taifa lenye uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za Umma.

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# MUHTASARI

Ripoti hii ina sura tisa zinazojumuisha kaguzi za Hesabu, Ukaguzi wa Kiufundi, Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA uliofanyika kwenye sekta mbalimbali za Umma katika mwaka wa fedha wa 2023/24. Maeneo yafuatayo yamejadiliwa kwa kina katika ripoti hii.

**Hati za Ukaguzi:** Nimetoa jumla ya hati 1,301 za Ukaguzi ikiwa ni ongezeko kutoka hati 1,291 mwaka 2022/23. Kati ya hati hizo Hati zinazoridhisha ni 1,295 (asilimia 99.5), Hati zenye shaka ni 5 (asilimia 0.4), Hati mbaya ni moja (asilimia 0.1) na hakukuwa na taasisi ambayo nimeshindwa kutoa maoni miongoni mwa Taasisi nilizozikagua kwa mwaka huu wa fedha. Kwa ujumla, hati za Ukaguzi wa hesabu zinaonesha utayarishaji unaoridhisha wa hesabu unaozingatia taratibu na kanuni za uandaaji wa hesabu.

**Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi:** Katika tathmini ya utekelezaji niliyofanya nimebaini kuwa kati ya mapendekezo 26,628 yaliyotolewa katika miaka iliyopita, mapendekezo 10,347 (asilimia 39) yametekelezwa kikamilifu, mapendekezo 10,433 (asilimia 39) utekelezaji wake unaendelea, mapendekezo 2,867 (asilimia 11) utekelezaji wake haujaanza, mapendekezo 1,984 (asilimia 7) yamerudiwa na mapendekezo 997 (asilimia 4) yamepitwa na wakati. Takwimu hizi zinaonesha kuwa, ingawa kuna maendeleo katika utekelezaji wa mapendekezo bado kuna nafasi ya kuboresha na kufanya vizuri zaidi.

Miongoni mwa masuala muhimu yaliyojitokeza ni pamoja na:

- Gharama za riba zinazoathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo - Shilingi Bilioni 71.47

- Ongezeko la Gharama Shilingi Bilioni 36.12 katika Utekelezaji wa Miradi
- Uwepo wa Dawa Zilizokwisha Muda na Zenye Muda Mfupi wa Matumizi- Shilingi Bilioni 12.44
- Uwekezaji wa Shilingi Bilioni 161.53 Usiozalisha Faida
- Matumizi yasiyo na Tija na Malipo yasiyo Halali – Shilingi Bilioni 378.17
- Miradi ya Ubia iliyosimama kwa Miaka 11 hadi 27 bila Kukamilika
- Matumizi yasiyo na Tija kwa Matengenezo ya Ndege 5H-MWF (Q300) - Shilingi Bilioni 20.63
- Kutotumika kwa Mifumo ya TEHAMA kwa Ufanisi
- Mapungufu ya mfumo wa MAJI-IS yaliyosababisha Kutokutozwa Ada za Matumizi ya Maji a Huduma za Maji Taka kwa Wateja
- Kukosekana kwa Kituo cha Kitaifa cha Usimamizi wa Usalama wa Mtandao (NSOC)
- Udhibiti Usioridhisha wa Vyombo Vya Usafiri Majini Vinavyomilikiwa na Serikali
- Upangaji na Uandaaji wa Bajeti usiotosheleza katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya Shughuli za Maandalizi ya kuzuia Mafuriko na Majanga Katika Maeneo Yao

SURA YA KWANZA




# Utangulizi

## 1.1 Utangulizi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi Kuu ya Ukaguzi nchini yenye jukumu la kukagua mapato na matumizi ya Serikali, kama yanavyoidhinishwa na Bunge na kutoa taarifa ya Ukaguzi Bungeni. Ofisi hii inaongozwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambaye majukumu yake yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (*kama ilivyorekebishwa*); Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 na Kanuni zake za Mwaka 2009 pamoja na Sheria nyingine.

## 1.2 Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali



## 1.3 Usimamizi wa Rasilimali za Taifa na Uwajibikaji

**Bunge**

Kuidhinisha na kusimamia mapato na matumizi ya Serikali pamoja na kutunga sheria za usimamizi za Umma

**Serikali**

Kukusanya na kutumia rasilimali za Taifa kama zilivyoidhinishwa na Bunge

**Mahakama**

Kutafsiri Sheria kwa kusikiliza mashauri yote yanayofikishwa Mahakamani na kutoa hukumu kulingana na sheria za nchi

## SURA YA PILI


# Hati za Ukaguzi wa Hesabu na Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi

## 2.1 Hati za Ukaguzi

Hati ni maoni ya Ukaguzi yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika Ukaguzi wa taarifa za fedha endapo zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu (kama vile IFRS au IPSAS).

Maoni haya hutolewa kwa kuzingatia tathmini ya vielelezo vinavyopatikana wakati wa Ukaguzi. Hati ya Ukaguzi hutolewa kwa mujibu wa Kiwango cha Kimataifa cha Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI) 1700. Kuna aina nne za Hati za Ukaguzi ikiwa ni Hati inayoridhisha, Hati yenye shaka, Hati mbaya na kushindwa kutoa maoni.

## Hati za Ukaguzi




## 2.2 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

Katika mwaka huu, nimetoa jumla ya hati 1,301 za Ukaguzi zikijumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Serikali Kuu, Miradi ya Maendeleo na Vyama vya Siasa. Mgawanyo wa Hati za Ukaguzi ni kama inavyoonekana hapo chini: -




Kwa ujumla utendaji wa Taasisi za Serikali katika kuandaa hesabu umeonesha matokeo mazuri, kwani asilimia 98 ya hati zote zilizotolewa zilionesha kuridhisha.

## 2.3 Taasisi zilizopata hati zenye shaka au hati mbaya

Jedwali Na. 1 linaonesha orodha ya Taasisi zilizopata hati zenye shaka au mbaya.

**Jedwali Na. 1: Taasisi zilizopata hati zenye shaka, mbaya na kushindwa kutoa maoni**

| Na. | Taasisi | Aina ya Hati |
|---|---|---|
| | **MASHIRIKA YA UMMA** | |
| 1 | Kiwanda cha Dawa cha Keko | Yenye shaka |
| 2 | Bodi ya Chai Tanzania | Yenye shaka |
| 3 | Chuo cha Sukari cha Taifa | Yenye shaka |
| 4 | Shirika la Posta Tanzania | Yenye shaka |
| | **MIRADI YA MAENDELEO** | |
| 5 | Halmashauri ya Wilaya ya Arusha (Mfuko wa Afya wa Pamoja) | Yenye shaka |
| | **VYAMA VYA SIASA** | |
| 6 | National Reconstruction Alliance (NRA) | Mbaya |

## 2.4 Utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi

Katika ripoti zilizopita, nilitoa mapendekezo kadhaa yaliyokusudia kuimarisha usimamizi wa rasilimali za Umma na kuboresha ukusanyaji wa mapato kama inavyoonekana hapo chini.





Ingawa kuna maendeleo katika utekelezaji wa mapendekezo bado kuna nafasi ya kuboresha katika maeneo mbalimbali. Asilimia 39 tu ya mapendekezo yote yametekelezwa kikamilifu na asilimia 39 bado yanaendelea kutekelezwa. Asilimia 11 ya mapendekezo hayajaanza kutekelezwa hata kidogo na asilimia 4 yamefutwa kwa sababu ya kupitwa na wakati.

## 2.5 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo Katika kaguzi za Ufanisi

Mchoro unaonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi 14 za ufanisi zilizowasilishwa Bungeni mwaka 2024.

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo katika kaguzi za ufanisi




Matokeo ya ufuatiliaji yanaonesha kuwa mapendekezo 213 yalitolewa katika kaguzi 14 za ufanisi zilizowasilishwa Bungeni Aprili 2021, ambapo hadi kufikia Disemba, 2024 mapendekezo 78 (sawa na asilimia 36.6) yalitekelezwa kikamilifu, mapendekezo 105 (sawa na asilimia 49.3) yaliyotolewa yametekelezwa kwa kiasi, wakati mapendekezo 29 (sawa na asilimia 13.6) hayakutekelezwa kabisa. Aidha pendekezo moja sawa na asilimia 0.5 lilikuwa limepitwa na wakati.

## SURA YA TATU




# Masuala ya Jumla na Hoja Mtambuka za Ukaguzi

### 3.1 Malimbikizo ya Madeni ya Taasisi za Umma Shilingi trilioni 7.23

Hadi tarehe 30 Juni 2024, taasisi 278 za Umma zilikuwa na madeni yasiyolipwa kwa zaidi ya miezi 12, yaliyofikia jumla ya Shilingi Trilioni 7.23. Hali hii imetokana na uhaba wa fedha, ucheleweshaji wa fedha kutoka Serikalini pamoja na utendaji dhaifu wa biashara za Taasisi husika. Kati ya deni hilo, Taasisi za mashirika ya Umma zinadaiwa Shilingi Trilioni 3.7, na Taasisi za Serikali Kuu zinadaiwa Shilingi Trilioni 3.53. Baadhi ya Taasisi hizo ni kama ifuatavyo.

**Jedwali Na. 2: Taasisi 12 zenye malimbikizo makubwa ya madeni**

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh. Bilioni) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | 1,179,927,226 | 16 |
| 2 | Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania | 1,028,938,589 | 14 |
| 3 | Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) | 1,006,021,455 | 14 |
| 4 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - (Fungu 57) | 904,794,956 | 13 |
| 5 | Shirika la Reli Tanzania (TRC) | 661,326,654 | 9 |
| 6 | Jeshi la Polisi - (Fungu 28) | 514,827,337 | 7 |
| 7 | Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) | 434,349,744 | 6 |
| 8 | Wizara ya Ujenzi - (Fungu 98) | 290,325,754 | 4 |
| 9 | Wakala wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RUWASA) | 198,412,566 | 3 |
| 10 | Wizara ya Afya - (Fungu 52) | 149,942,498 | 2 |
| 11 | Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) | 132,805,704 | 2 |

| Na. | Taasisi | Kiasi (Sh. Bilioni) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 12 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) - (Fungu 38) | 112,979,665 | 2 |

### 3.2 Usimamizi Duni wa Mali zilizotelekezwa - Shilingi Bilioni 37.07

Ukaguzi umebaini magari 552, pikipiki 98 na mashine 20 hazitumiki kwa muda mrefu katika Taasisi 81 bila hatua za matengenezo au uuzaji kutokana na ucheleweshaji wa maamuzi na ukosefu wa mipango. Pia majengo na mitambo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 37.07 hayatumiki, ikiwemo jengo la IPS (miaka mitatu), mitambo ya Bohari ya Dawa tangu 2020/21 na baadhi ya majengo ya utalii kwenye hifadhi za Taifa.

Hali hii imesababishwa na ukosefu wa fedha za ukarabati, ucheleweshaji wa manunuzi na ukosefu wa mpango wa matumizi hivyo kusababisha hasara na kuathiri huduma kwa wananchi.

### 3.3 Uwepo wa Dawa zilizokwisha Muda na Zenye Muda Mfupi wa Matumizi- Shilingi Bilioni 12.44

Ukaguzi umebaini dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 12.44 vimeharibika kutokana na kuisha muda wa matumizi bila kuondolewa. Sababu kuu ni ucheleweshaji wa vibali vya kisheria vya kuziondoa, ununuzi wa dawa bila tathmini ya mahitaji na kutofuata utaratibu wa Kile kilichoingia kwanza, ndicho kinachotumika au kuuzwa kwanza. Hali hii imeongeza gharama za uhifadhi na kuhatarisha usalama wa watumiaji.

**Jedwali Na. 3: Taasisi zenye Dawa zilizokwisha muda**

| Taasisi | Thamani ya Dawa (Shilingi Bilioni) | Maelezo |
|---|---|---|
| Bohari Kuu ya Dawa | 4.18 | Dawa zilizokwisha muda wa matumizi |
| Bohari Kuu ya Dawa | 4.86 | Dawa zenye muda mfupi wa matumizi (chini ya miezi 6) |
| Hospitali ya Taifa Muhimbili | 0.157 | Dawa zilizokwisha muda wa matumizi |
| Hospitali ya Taifa Mloganzila | 0.108 | Dawa zilizokwisha muda wa matumizi |
| Hospitali 11 kati ya 34 za Rufaa za Mikoa | 1.41 | Dawa zilizokwisha muda hadi miaka 5; Tabora RRH ilikuwa na dawa zenye thamani ya Shilingi milioni 619.25 (43% ya jumla) |
| Halmashauri 13 | 1.73 | Dawa zilizokwisha muda hadi miaka 10; H/wilaya Maswa ilikuwa na dawa zenye thamani ya Shilingi milioni 765.71 (44% ya jumla) |
| **Jumla** | **12.445** | |

## 3.4 Malimbikizo ya Madeni ya Watumishi Shilingi Bilioni 311.98

Ukaguzi umebaini Taasisi 269 za Umma zinadaiwa jumla ya Shilingi Bilioni 311.98 za madeni ya watumishi, ikijumuisha Serikali Kuu (Shilingi Bilioni 274.8 - asilimia 88), Mamlaka za Serikali za Mitaa (Shilingi Bilioni 24.54 - asilimia 8), na Mashirika ya Umma (Shilingi Bilioni 12.64 - asilimia 4). Madeni haya ni ya mishahara, gharama za usafiri kwa wastaafu na marupurupu mbalimbali. Sababu kuu ni ufinyu wa bajeti, ucheleweshaji wa fedha na udhaifu katika usimamizi wa fedha za Umma.

SURA YA NNE



# Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu

## 4.1 Mwenendo wa deni la Serikali

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, deni la Serikali lilifikia kiasi cha Shilingi Trilioni 97.36, kutoka Shilingi Trilioni 82.25 mwaka uliopita sawa na ongezeko la Shilingi Trilioni 15.10 (asilimia 18). Deni hili linajumuisha deni la ndani Shilingi Trilioni 31.95 na deni la nje Shilingi Trilioni 65.41.

Kwa mujibu wa Tathmini ya Uhimilivu wa Deni ya Desemba 2024, deni la Serikali bado ni himilivu ambapo uwiano wa deni kwa Pato la Taifa la ndani (asilimia 41.1) na deni la nje kwa Pato la Taifa (asilimia 23.6) upo chini ya viwango vya juu vinavyokubalika (asilimia 55 na asilimia 40 mtawalia).



## 4.2 Athari za Kutoweka Masharti ya Kulinda Haki za Kisheria katika Marekebisho ya Sheria ya Madini na Maliasili


Marekebisho ya Sheria ya Madini na Maliasili (2017) hayakuzingatia haki zilizokuwepo chini ya Sheria ya Madini (2010), na hivyo kusababisha Serikali kushitakiwa kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Uwekezaji (ICSID) na kulipa fidia ya Shilingi Bilioni 74.88 kwa kampuni ya Winshear Gold Corporation.

Serikali pia bado inakabiliwa na kesi zenye madai ya Dola Milioni 159.40 za Marekani (Nachingwea Nickel, milioni 90; Montero Mining, milioni 69.4). Kukosekana kwa tathmini ya athari za kisheria kabla ya mabadiliko haya kumesababisha hasara kubwa na kudhoofisha mazingira ya uwekezaji wa Kimataifa.

## 4.3 Upotevu wa Lita 14,459,706.19 za Mafuta yanayosafirishwa Kupitia Bomba la TAZAMA

Ukaguzi wa mafuta yaliyosafirishwa kupitia bomba la TAZAMA (Januari 2023 – Agosti 2024) ulibaini upungufu wa lita milioni 14.46 zenye kodi ya Shilingi bilioni 12.6 ambazo hazikufika kituo cha Inyala, Mbeya, kinyume na Kanuni za Forodha za Jumuiya ya Afrika Mashariki (2010).

Hali hii inaashiria kuwa mafuta hayo huenda yalibaki nchini bila kulipiwa kodi kinyume cha sheria na hivyo kusababisha upotevu wa mapato na kudhoofisha udhibiti wa forodha.




## 4.4 Udhaifu Katika Uhakiki wa Mkataba Uliosababisha Hasara ya Shilingi Bilioni 13.72

TANROADS ilisaini mkataba wa Shilingi bilioni 38.36 (Desemba 2022) kwa miradi mitatu ya barabara mkoani Songwe: Ibanda-Kajunjumele (km 22), Kajunjumele–Bandari ya Kiwira (km 6) na Kajunjumele–Bandari ya Itungi (km 4). Hata hivyo, mkandarasi alicheleweshа kazi na kutoa nyaraka za kughushi, ikiwemo dhamana kutoka benki ya Azerbaijan ambayo imefilisika na haiwezi kulipa.

Mei 2024, TANROADS ilisitisha mkataba na kuanza taratibu za kudai kurejeshewa Shilingi bilioni 13.72, lakini suala hili limepelekwa kwenye usuluhishi baada ya mkandarasi kupinga madai hayo. Hali hii inahatarisha urejeshwaji wa fedha za Umma na kuchelewesha huduma bora kwa wananchi.




## 4.5 Upungufu wa Bajeti ya Shilingi Trilioni 1.43 kwa Matengenezo ya Barabara

Ukaguzi umebaini pengo kubwa la bajeti la Shilingi Trilioni 1.43 katika matengenezo ya barabara kwa mwaka 2023/24, hali inayohatarisha ujenzi endelevu wa miundombinu nchini. Ingawa TANROADS na TARURA zinahitaji Shilingi Trilioni 2.29 kwa matengenezo, bajeti iliyotengwa ni Shilingi bilioni 856.79 pekee, huku kiasi halisi kilichotolewa kilikuwa Shilingi 405.29 ambazo ni  asilimia 47 tu ya bajeti hiyo.

Hii imesababisha upungufu mkubwa wa fedha licha ya kuongezeka kwa mapato ya ushuru wa mafuta na ada za magari ya kimataifa. Kutokubuni vyanzo vipya vya mapato na kutopitiwa kwa bajeti kunaongeza hatari ya uharibifu zaidi wa barabara, ongezeko la gharama za ukarabati siku zijazo na kuathiri ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi.

## 4.6 TEMESA Kuendesha Vivuko Bila Vyeti vya Usalama

TEMESA inaendesha vivuko 32 bila Cheti cha Usalama kutoka TASAC kutokana na tafsiri kinzani ya Sheria ya Usafiri wa Meli na Kanuni zake kuhusu hitaji la bima kwa vyombo vya Serikali. Mfano, vivuko vya MV Magogoni na MV Kigamboni vinatoa huduma bila uthibitisho wa usalama. Hali hii inahatarisha usalama wa abiria na wafanyakazi kwani vyombo hivyo havijakaguliwa kuthibitisha ustahili wa safari baharini.

## 4.7 Gharama Kubwa za Kulipa Kodi ya Pango katika Balozi za Tanzania Nje ya Nchi

Katika mwaka wa fedha 2023/24, balozi 39 kati ya 43 zilitumia Shilingi bilioni 22.63 kulipia kodi ya Ofisi na makazi, sawa na asilimia 14 ya bajeti. Kwa miaka mitatu mfululizo, jumla ya Shilingi Bilioni 56.56 zilitumika kwa malipo hayo, fedha ambazo zingeweza kujenga au kukarabati majengo ya balozi kama kungekuwepo utaratibu wa mikopo kwa ujenzi.

Gharama hizi zimesababishwa na Serikali kushindwa kuendeleza viwanja au kukarabati majengo chakavu ya balozi. Hali hii inapunguza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kidiplomasia.

SURA YA TANO



# Ukaguzi wa Tawala za Mi na Serikali za Mitaa

## A. UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA BAJETI

### 5.1 Bajeti Duni na Mpango Hafifu wa Kulipa Madeni – Shilingi Bilioni 70.2

Ukaguzi wa bajeti za Halmashauri kwa mwaka 2023/24 ulibaini kuwa halmashauri 43 na sekretarieti 2 za mikoa hazikutenga fedha za kutosha kulipa madeni ya Shilingi Bilioni 70.2 kwa wazabuni na watumishi kinyume na Mwongozo wa Bajeti wa 2023/24.

Kutolipa madeni haya kumesababisha ongezeko la gharama za riba, kudhoofisha utendaji wa wazabuni, kuchelewesha huduma kwa wananchi, kupunguza ari ya watumishi na kuharibu taswira ya halmashauri mbele ya wadau.

## B. USIMAMIZI WA MAPATO

Katika mwaka wa fedha 2023/24, mamlaka za Serikali za mitaa zimekusanya jumla ya Shilingi Trilioni 1.23, ambayo ni zaidi ya makisio ya Shilingi Trilioni 1.14. Ongezeko hili ni Shilingi Bilioni 87.75 sawa na asilimia 8. Halmashauri 110 zilivuka malengo yao ya makusanyo kwa Shilingi Bilioni 155.39, huku halmashauri 72 zikishindwa kufikia malengo kwa jumla ya Shilingi Bilioni 74.82.

Matokeo haya yanaonesha umuhimu wa kupanga bajeti halisi na kuimarisha mikakati ya ukusanyaji mapato ili kuhakikisha uendelevu wa kifedha katika Serikali za mitaa.

## 5.2 Tofauti Kubwa Kati ya Mikataba na Makusanyo Halisi ya Mawakala

Katika mwaka wa fedha 2023/24, mamlaka 14 za Serikali za mitaa zilitarajiwa kukusanya Shilingi Bilioni 45.61 kupitia mawakala wa mapato, lakini zikakusanya Shilingi Bilioni 19.49, zikileta pungufu ya Shilingi Bilioni 26.12. Pungufu kubwa zaidi, inayozidi Shilingi Bilioni 1, ilitambuliwa katika halmashauri sita. Taarifa ya kina inapatikana katika jedwali linalofuata:

**Jedwali Na. 4: Mamlaka za Serikali za mitaa zilizokusanya mapato bila kuzingatia matakwa ya mkataba**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi kilichotakiwa kukusanywa (Shilingi) | Kiasi kilichokusanywa (Shilingi) | Kiasi ambacho hakijakusanywa (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dar es Salaam | 15,000,000,000 | 3,479,778,733 | 11,520,221,267 |
| 2 | H/M Kinondoni | 9,306,336,000 | 5,516,784,717 | 4,739,951,283 |
| 3 | H/M Ubungo | 3,120,000,000 | 909,779,440 | 2,210,220,560 |
| 4 | H/Jiji Mwanza | 3,652,299,719 | 1,643,585,916 | 2,008,713,803 |
| 5 | H/W Kibondo | 2,191,250,000 | 635,604,400 | 1,555,645,600 |
| 6 | H/W Babati | 2,500,975,000 | 1,447,145,753 | 1,053,829,247 |




## 5.3 Fedha Zilizokusanywa lakini Hazikuwekwa Benki

Ukaguzi ulibaini kuwa Halmashauri 37 zilikusanya Shilingi Bilioni 3.45 ambazo hazikuwekwa kwenye akaunti rasmi za Serikali. Hali hii inaashiria uwezekano wa ubadhirifu wa fedha za Umma na kusababisha ucheleweshaji wa utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi.

**C. SEKTA YA UWEKEZAJI TAMISEMI NA MAMLAKA ZA SERIKALI YA MITAA**

## 5.4 Kushindwa kwa UDART Kufikia Viwango vya Utendaji na Athari kwenye Ubora wa Huduma

Ukaguzi umebaini kuwa watoa huduma wa Mabasi Yaendayo Haraka (UDART) hawajazingatia viwango vya utendaji vilivyokubalika kimkataba, ikiwemo kushindwa kuhakikisha asilimia 90 ya mabasi yanatoa huduma wakati wa msongamano mkubwa, kudhibiti muda wa safari na kutunza ubora wa mabasi na huduma kwa abiria.

Kutokana na hilo, hadi Juni 2024 makato na adhabu za kifedha zilifikia Shilingi Bilioni 15.32, huku faini za mwaka 2023/24 pekee zikiongezeka kwa asilimia 27 sawa na Shilingi Bilioni 3.84. Hii imetokana na usimamizi dhaifu na kukosekana kwa mfumo wa kisasa wa kufuatilia huduma (Intelligent Transport System - ITS), na kusababisha kupungua kwa ubora wa huduma, malalamiko kutoka kwa abiria na hatari ya Mamlaka ya DART kupoteza mapato.

## 5.5 Upungufu wa Mabasi ya UDART Unaosababisha Huduma Duni za Usafiri

Mkataba wa huduma kati ya DART na UDART unahitaji mabasi 210 yafanye kazi, lakini hadi tarehe 22 Novemba 2024, mabasi 111 pekee ndiyo yalikuwa yanatumika, huku 99 yakiwa hayafanyi kazi kutokana na uchakavu, ajali, na kuhitaji matengenezo.

Upungufu huu wa asilimia 49 umeongeza msongamano, kuchelewesha safari na kuathiri ubora wa huduma kwa wasafiri. Tatizo limechangiwa na ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara hali inayokiuka mkataba wa uendeshaji wa mabasi.

## 5.6 Kushuka kwa Thamani ya Uwekezaji wa Hisa katika DCB Bank

Katika mwaka 2023/24, uwekezaji wa Halmashauri za Jiji na Manispaa za Dar es Salaam kwenye hisa za Benki ya DCB ulishuka thamani kutoka Shilingi Bilioni 4.47 hadi Shilingi Bilioni 3.51, na kusababisha hasara ya Shilingi Milioni 957.72.

Thamani ya hisa moja ilipungua kutoka Shilingi 140 mwaka 2023 hadi Shilingi 110 mwaka 2024, ikiwa ni mwaka wa tatu mfululizo wa kushuka bila mgawanyo wowote wa faida.


Kukosekana kwa tathmini na mpango madhubuti wa uwekezaji kunahatarisha upotevu zaidi wa fedha za Umma.

## D. USIMAMIZI WA MALI SERIKALI ZA MITAA

### 5.7 Kutotumika kwa Vifaa vya Matibabu kutokana na Ukosefu wa Miundombinu, Wataalamu na Vipuri

Vifaa vya matibabu vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 3.85 katika vituo vya afya 25 havitumiki kutokana na ukosefu wa wataalamu, miundombinu duni, majengo kutokamilika na uhaba wa vitendanishi vya maabara (reagents).

Pia, vifaa 65 ikiwemo mashine za X-ray na za kufulia katika hospitali sita havijafanya kazi kwa zaidi ya miaka miwili kutokana na kukosekana kwa miundombinu inayohitajika pamoja na vipuri, hali inayosababisha upotevu wa fedha na hatari ya uchakavu kabla ya kutumika ipasavyo.




### 5.8 Miradi ya Ujenzi Iliyokamilika Lakini Haitumiki Shilingi Bilioni 5.64

Ukaguzi wangu wa miradi ya ujenzi (2023/24) umebaini miradi 45 ya afya, elimu na utawala yenye thamani ya Shilingi Bilioni 5.64 katika mamlaka 11 za Serikali za mitaa imekamilika lakini haitumiki. Sababu kuu ni upungufu wa watumishi, ukosefu wa samani, vifaa vya maabara, vyoo na miundombinu mingine muhimu.

Hali hii inaathiri utoaji wa huduma, inaongeza gharama za matengenezo na kuhatarisha uchakavu kabla ya miradi hiyo kutumiwa.

**Jedwali Na. 5: Halmashauri zenye miradi iliyokamilika lakini haitumiki**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Miradi | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Mkuranga | 12 | 2,486,907,918 |
| 2. | H/W Misungwi | 7 | 728,661,050 |
| 3. | H/W Ileje | 2 | 608,000,000 |
| 4. | H/W Itigi | 3 | 500,000,000 |
| 5. | H/M Temeke | 2 | 449,293,900 |
| 6. | H/W Chemba | 5 | 230,000,000 |
| 7. | H/W Mbulu | 4 | 215,115,740 |
| 8. | H/W Mkinga | 2 | 114,400,000 |
| 9. | H/Mji Mbulu | 5 | 108,000,000 |
| 10. | H/W Mvomero | 1 | 100,000,000 |
| 11. | H/Mji Geita | 2 | 95,000,000 |
| **Jumla** | | **45** | **5,635,378,608** |

## E. SEKTA YA AFYA

### 5.9 Kutofikiwa kwa Lengo la iCHF la Uandikishaji wa Kaya

Waraka Na. 1 wa Ofisi ya Rais TAMISEMI (2018) uliagiza Sekretarieti za Mikoa kuhamasisha uandikishaji wa kaya mpya kwenye bima ya afya iliyoboreshwa (iCHF). Hata hivyo, Sekretarieti 17 za Mikoa hazikufikia malengo, ambapo hadi Juni 2024 kaya 159,773 tu kati ya 1,247,474 zilijiunga.

Sababu kuu ni huduma duni za afya zikilinganishwa na NHIF, changamoto za kiufundi za mfumo wa IMIS na baadhi ya maofisa waandikishaji kujitoa katika ngazi za kata na vijiji. Hali hii inahatarisha mafanikio na uendelevu wa mfuko huo.

### 5.10 Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Dawa na Vifaa vya Tiba Kuelekezwa kwenye Matumizi Mengine Shilingi Bilioni 4.75

Aya ya 3.2(i) ya Maelekezo ya Wizara ya Afya (2017) kuhusu Usimamizi wa Mfuko wa Uchangiaji Gharama inataka asilimia 50 ya makusanyo ya papo kwa papo (user fee) itumike kununua dawa na vifaatiba.

Hata hivyo, tathmini katika halmashauri 10 ilibaini kuwa kati ya Shilingi Bilioni 17.55 zilizokusanywa, Shilingi Bilioni 8.78 zilipaswa kutengwa kwa vifaatiba, lakini kiasi cha Shilingi Bilioni 4.44 kilielekezwa kwenye matumizi mengine kama posho na matumizi ya kawaida. Hali hii inadhoofisha juhudi za kuboresha huduma za afya na inapunguza ubora wa huduma kwa wananchi.

## F. SEKTA YA ARDHI

### 5.11 Kutotolewa kwa Hatimiliki kwa wanufaika wa Viwanja 1975 Vilivyolipiwa Kikamilifu Vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 6.59

Sheria ya Ardhi (Sura ya 113, Kifungu 29(1) inaitaka mamlaka husika kutoa hatimiliki kwa wamiliki wa ardhi. Hata hivyo, licha ya Manispaa ya Kigamboni kupima na kuuza viwanja 2,220 vilivyolipiwa kikamilifu kufikia mwaka 2021/22, hadi Novemba 2024 ni wanufaika 245 pekee waliopata hatimiliki.

Viwanja 1,975 (asilimia 89) vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 6.59 havina hatimiliki kutokana na wanunuzi kutowasilisha nyaraka muhimu kama vitambulisho vya NIDA, uwasilishaji usiokamilika wa fomu Na. 19, na ucheleweshaji wa kurejesha hatimiliki kutoka kwa mmiliki wa awali wa eneo la Pembamnazi-Tundwi Songani. Hii imeathiri haki ya umiliki na maendeleo ya maeneo hayo.

SURA YA SITA




# Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma

## A. UTENDAJI WA KIFEDHA WA MASHIRIKA YA UMMA

### 6.1 Taasisi zilizopata hasara au nakisi

Katika mwaka 2023/24, mashirika 31 ya Umma yalipata faida, yakiongozwa na TPDC (Shilingi Bilioni 248.75), NHC (Shilingi Bilioni 242.90) na TPA (Shilingi Bilioni 140.48). Hata hivyo, baadhi ya mashirika yaliendelea kupata hasara kutokana na changamoto za kiutendaji na kiuongozi:




- **Shirika la Reli (TRL)** lilipata hasara ya Shilingi Bilioni 224 kutokana na kupungua kwa mapato ya usafirishaji

kwa sababu ya uhaba wa vichwa vya treni na mabehewa, pamoja na kufungwa kwa njia kutokana na mvua kubwa. Hasara hii ni kabla ya kuanza kwa huduma za usafirishaji wa treni ya abiria (SGR).

- **Kampuni ya Ndege (ATCL)** ilipata hasara ya Shilingi Bilioni 91.8 kutokana na gharama kubwa za matengenezo ya ndege, hitilafu za injini na ucheleweshaji wa huduma za mizigo.
- **TTCL** ilipata hasara ya Shilingi Bilioni 27.78 kutokana na kuongezeka kwa gharama baada ya kuhamishiwa Mkongo wa Taifa na Kituo cha Taifa cha Data, huku mapato ya mkongo yakiwasilishwa moja kwa moja Serikalini badala ya shirika.
- **Shirika la Posta** lilipata hasara ya Shilingi Bilioni 23.63 kutokana na kupungua kwa mapato kwa asilimia 20 na ongezeko la gharama za uendeshaji kwa asilimia 46.
- **Shirika la Masoko ya Kariakoo** lilipata hasara ya Shilingi Bilioni 1.45 kutokana na uharibifu wa jengo uliochangiwa na moto.
- **Soko la Bidhaa Tanzania** lilipata hasara ya Shilingi Milioni 561.92 kutokana na ada ndogo au kutotozwa kwa baadhi ya bidhaa pamoja na ongezeko la gharama za uendeshaji kwa asilimia 17.




Hasara hizi zilisababisha Serikali kutoa ruzuku kubwa za uendeshaji, hali inayohitaji hatua za haraka ili kuongeza ufanisi na tija katika mashirika hayo.

## B. MWENENDO WA BENKI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI

### 6.2 Usimamizi Duni wa Dhamana Zilizowekwa

Ukaguzi wa usimamizi wa mikopo katika benki tatu umebaini mapungufu makubwa katika usimamizi wa dhamana. Benki ya Maendeleo ya TIB ilitoa mikopo ya Shilingi Bilioni 209.05 kwa dhamana za Shilingi Bilioni 52.06 pekee, na hivyo kusababisha upungufu wa Shilingi Bilioni 156.99. Aidha, dhamana za Shilingi Bilioni 19.63 zilikuwa zimepita muda wa matumizi.

Katika Benki ya TCB, mikopo 31 (Shilingi Bilioni 24.93) haikuwa na ripoti za uthamini, mikopo 6 (Shilingi Bilioni 20.31) ilikuwa na dhamana zisizo na bima, na dhamana za mikopo 13 (Shilingi Bilioni 47.14) hazikuhakikiwa kikamilifu.

Kwa Benki ya Azania, kulikuwa na tofauti ya Shilingi Bilioni 277.07 kati ya rejista ya dhamana (Shilingi Bilioni 786.27) na nyaraka za uthibitisho zilizopo (Shilingi Bilioni 509.20), ikionyesha udhaifu katika utunzaji kumbukumbu.

Mapungufu haya yametokana na usimamizi duni wa dhamana na ukosefu wa maridhiano ya mara kwa mara ya kumbukumbu na nyaraka za dhamana hizo.

## 6.3 Utendaji Duni wa Kampuni ya TIB Rasilimali Limited

Kampuni ya TIB Rasilimali Limited haijapata faida kwa zaidi ya miaka mitano, ambapo mwaka 2024 ilipata hasara ya Shilingi Milioni 539.86, kutoka Shilingi Milioni 343.80 mwaka 2022. Kufikia Desemba 2024, kampuni ilikuwa na deni lililozidi mali zake kwa Shilingi Bilioni 1.25 na hasara iliyokusanywa ya Shilingi Bilioni 3.63. Sababu kuu ni ukosefu wa mtaji wa kutosha na mabadiliko ya wawekezaji kutoka hisa kwenda hati fungani zenye riba.






### 6.4 Ukosefu wa Mtaji wa Kutosha wa Benki ya Maendeleo ya TIB - Shilingi Bilioni 112.74

Benki ya Maendeleo ya TIB ilikuwa na upungufu wa mtaji wa Shilingi Bilioni 112.74, kwani mtaji wake ulikuwa Shilingi Bilioni 87.26 badala ya kiwango cha kisheria cha Shilingi bilioni 200. Benki bado inasubiri nyongeza ya mtaji kutoka Wizara ya Fedha.

Aidha, hadi Machi 2025 benki ilikuwa na deni la Shilingi Bilioni 37 kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina (OTR) tangu 2019, na madeni mengine ya muda mrefu ya Shilingi Bilioni 183 kutoka kwa wadai mbalimbali, huku mali zake zikiwa Shilingi Bilioni 2.84 pekee.

### 6.5 Usimamizi Usioridhisha wa Mfuko wa SELF

Mfuko wa SELF ulitoa mikopo kwa riba ya asilimia 24 badala ya asilimia 30 kinyume na miongozo ya mwaka 2023, pamoja na kutokutumia kanuni sahihi ya kukokotoa riba. Aidha, mkopo mmoja wa Shilingi Milioni 79 ulitolewa kinyume na matumizi yaliyokubaliwa, na mkopaji alishindwa kurejesha fedha hizo. Usimamizi na uchambuzi dhaifu umeongeza hatari ya mikopo isiyolipika.

## C. UFANISI WA MASHIRIKA YA UMMA KATIKA UTENDAJI KAZI

### 6.6 Madeni ya TANESCO kwa IPTL na Urejeshaji wa Fedha za Tegeta Escrow

TANESCO inadaiwa Shilingi Bilioni 238.71 na IPTL, ikijumuisha deni halisi la Shilingi Bilioni 111.48 na riba ya Shilingi Bilioni 127.22 kutokana na kuchelewesha malipo kati ya mwaka 2009

hadi 2017. Aidha, IPTL imewasilisha madai mengine ya fidia, gharama za uzalishaji na ada za kisheria licha ya TANESCO kudai mgogoro huo ulimalizwa kupitia Kesi Na. 200 ya mwaka 2015. Pia, IPTL bado haijarejesha Dola milioni 148.4 za Marekani (Shilingi Bilioni 389.83) inazodaiwa na Serikali kutokana na matumizi mabaya ya fedha za Tegeta Escrow tangu Februari 2022.

### 6.7 Mikopo Isiyorejeshwa ya Shilingi Trilioni 1.29

Mifuko ya hifadhi ya jamii bado inakabiliwa na changamoto ya mikopo ya muda mrefu isiyorejeshwa kutoka kwa mashirika ya Umma. Hadi Juni 2024, NSSF ilikuwa inadai Shilingi Trilioni 1.06 (imeshuka kutoka Trilioni 1.50), na PSSSF ilidai Shilingi Bilioni 231.4 bila mabadiliko kwa miaka miwili mfululizo. Mikopo hii haijalipwa kwa kipindi cha hadi miaka 17.

### 6.8 Ucheleweshaji wa Fidia kwa Wafanyakazi Walioumia Kazini Shilingi Milioni 262.70

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi umechelewesha kushughulikia madai 23 kati ya 28 kwa wastani wa siku 82, kinyume na mwongozo wa siku 30 hadi 60. Jumla ya madai ya fidia yaliyochelewa ni shilingi Milioni 262.7. Ucheleweshaji huu unaathiri familia za wafanyakazi na kuzidisha matatizo ya kijamii.

### 6.9 Uwekezaji wa Shilingi Bilioni 161.53 Usiozalisha Faida

PSSSF imewekeza Shilingi Bilioni 161.53 katika vitega uchumi vinane ikiwemo Kampuni ya Majengo ya Biashara ya Jiji la Mwanza (Shilingi Bilioni 72), Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro (Shilingi Bilioni 59.96) ambavyo havijazalisha faida kwa kipindi cha hadi miaka saba. Hii

inakiuka Mwongozo wa Benki Kuu unaotaka kila uwekezaji uzalishe faida inayozidi amana ya Serikali. Baadhi ya vitega uchumi hivi havina mkakati wa namna ya kuviondoa licha ya kutoleta tija.




## 6.10 Mwenendo wa Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania (TCPM)

Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania (TCPM), kampuni tanzu ya TANESCO iliyoanzishwa ili kuzalisha na kupima ubora wa nguzo za zege nchini, haijatekeleza majukumu yake ipasavyo kwa zaidi ya miaka 10 tangu kuanzishwa kwake. Katika mwaka 2023/24, TCPM ilipokea Shilingi Bilioni 6 kutoka TANESCO, lakini fedha nyingi zilitumika kwenye gharama za kawaida na kulipa wazabuni wa nje badala ya kujenga kiwanda na maabara yake yenyewe. Kutokana na hali hiyo, kampuni inaendelea kutegemea huduma za nje. Inapendekezwa kampuni hii ama ifanywe kuwa idara ndani ya TANESCO au ipewe rasilimali za kutosha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

## D. USIMAMIZI WA RASILIMALI NA MALI

### 6.11 Matumizi Yasiyo na Tija na Malipo Yasiyo Halali - Shilingi Bilioni 378.17

Kwa mwaka 2023/24, Ukaguzi umebaini matumizi yasiyo na tija na malipo yasiyo halali yenye thamani ya Shilingi Bilioni 378.17 katika taasisi za Umma. Matumizi yasiyo na tija (Shilingi Bilioni 371.42) yalitokana na riba na faini za ucheleweshaji kodi, michango ya pensheni, mishahara kwa watumishi waliosimamishwa bila kibali, na ucheleweshaji wa malipo kwa wazabuni. Mfano:

- Mamlaka ya Bandari (TPA): Shilingi Bilioni 17.35 za faini na riba za kodi.
- Chuo Kikuu cha Muhimbili (MUHAS): Shilingi Milioni 31.89 za faini za pensheni.
- Bodi ya Nafaka: Shilingi Milioni 370.63 za mishahara kwa watumishi waliosimamishwa bila kibali.

Malipo yasiyo halali (Shilingi Bilioni 6.75) yalihusisha mishahara na posho zisizoidhinishwa. Mfano:

- Bodi ya Nafaka: Shilingi Bilioni 2.05 mishahara bila kibali.
- TANESCO: Shilingi Bilioni 2.04 mishahara kwa wastaafu na posho zisizoidhinishwa.
- ATCL: Shilingi Bilioni 1.32 posho zilizozidi viwango vilivyoidhinishwa.

Hali hii imesababisha ongezeko la madeni, kupoteza fedha za maendeleo, na kuonyesha mapungufu katika uwajibikaji wa fedha za Umma.

## 6.12 Matumizi Yasiyo na Tija kwa Matengenezo ya Ndege 5H-MWF (Q300) - Shilingi Bilioni 20.63

Ndege aina ya DASH 8 Q300 (5H-MWF) haijafanya kazi kwa zaidi ya miaka saba, huku karibu miaka minne ikiwa katika matengenezo yasiyo na mafanikio tangu ilipopelekwa Nchini Malta Novemba 2020. Licha ya Shilingi Bilioni 20.63 kutumika kwa matengenezo na bima tangu 2020, ndege hii bado haijaanza kufanya kazi hadi tarehe 30 Juni 2024, bila mpango maalum wa kurejeshwa kwenye huduma. Sababu kuu za tatizo hili ni kushindwa kufanya tathmini ya kiuchumi kabla ya kuanza matengenezo.

## E. MADAI

## 6.13 Malimbikizo ya Madai ya Taasisi za Umma – Shilingi Trilioni 3.58

Ukaguzi umebaini Taasisi 106 za Umma zina madai ya muda mrefu ya Shilingi Trilioni 3.58, kutoka Shilingi Trilioni 2.92 mwaka uliopita. Baadhi ya madai hayo ni:

- NHIF inadai Shilingi Bilioni 180 kutoka Taasisi nne za Serikali.
- MSD inadai Serikali Shilingi Bilioni 267.79, ongezeko la asilimia 14.
- Bodi ya Mikopo (HESLB) inadai Shilingi Bilioni 931.14 za mikopo ya wanafunzi, ongezeko la asilimia 15.
- Shirika la Nyumba (NHC) linadai Shilingi Bilioni 19.09 za kodi kutoka wapangaji waliotoroka.

- Hospitali ya Muhimbili inadai Shilingi Bilioni 20.88 baada ya kutoa huduma kwa wadaiwa sugu, kinyume na sera yake.
- TTCL inadai Shilingi Bilioni 102.42 kutoka wateja wa Serikali na binafsi.
- Mfuko wa Mafunzo ya Usafiri wa Anga unadai Shilingi Bilioni 19.42 kutokana na ucheleweshaji wa michango.

Hali hii inadhoofisha uwezo wa Taasisi hizi kutoa huduma bora kwa Umma.

## F. USIMAMIZI WA MIRADI NA MANUNUZI

### 6.14 Miradi ya Ubia Iliyosimama kwa Miaka 11 hadi 27 Bila Kukamilika

Ukaguzi umebaini kuwa miradi 24 ya ubia ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) imekwama kwa kati ya miaka 11 hadi 27, licha ya mikataba kutaka ikamilike ndani ya miaka mitatu. Licha ya changamoto hizo, mwaka 2023/24, NHC imesaini mikataba mingine 20 ya ubia, na hivyo kuongeza miradi isiyoleta faida.

Udhaifu wa usimamizi umesababisha mali za shirika (ardhi, majengo, na fedha) kufungiwa kwenye miradi isiyozalisha na hivyo kuhatarisha ufanisi na maendeleo ya shirika hilo.




### 6.15 Malipo ya Awali Yanayohatarisha Hasara ya Shilingi Bilioni 7.51

Mnamo Julai 2017, TANESCO iliingia mkataba wa Shilingi Bilioni 33.68 kwa ajili ya vifaa vya usambazaji umeme, na kufanya malipo ya awali ya Shilingi Bilioni 6.73. Hata hivyo, hadi Oktoba 2024 (miaka saba baadaye), vifaa hivyo havijawasilishwa, na hivyo kuhatarisha upotevu wa fedha hizo.

Pia, hadi Juni 2024, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kilifanya malipo ya awali ya Shilingi Milioni 783.25 kwa vifaa vya Ofisi ambavyo havikupokelewa kwa zaidi ya miezi 12, hali inayoathiri huduma na kuhatarisha upotevu wa fedha za Umma.

### 6.16 Malipo ya Awali Bila Kuzingatia Taratibu - Shilingi Bilioni 3.66

Ukaguzi katika mashirika sita umebaini malipo ya awali yasiyo na udhibiti yenye thamani ya Shilingi Bilioni 3.66. Chuo cha

Uhasibu Arusha, Kituo cha Zana za Kilimo na Kampuni ya Sisalana zilifanya malipo ya Shilingi Milioni 989 bila dhamana za wazabuni. Aidha, Hospitali ya Muhimbili ililipa Shilingi Milioni 71 kwa mradi ulioachwa bila kurejesha fedha, na Chuo cha Uhasibu kililipa Shilingi Milioni 324 kwa gari ambalo halijawasilishwa.

STAMIGOLD ililipa Shilingi Milioni 148 bila kupokea bidhaa, huku wasambazaji wengine wakikataa kuwasilisha bidhaa baada ya kupokea Shilingi milioni 74 kutokana na madeni ya nyuma. TANESCO nayo haikuongeza muda wa dhamana ya Shilingi Bilioni 2.13 kwa mradi wa kituo cha umeme Ununio baada ya kuisha muda wake.

Hali hii imeweka fedha za Umma katika hatari ya kupotea kutokana na usimamizi dhaifu wa malipo ya awali na udhibiti wa mikataba.

## 6.17 Changamoto Katika Utekelezaji wa Mradi wa Kawe 711 na Madai ya Shilingi Bilioni 49.04

Mradi wa ujenzi wa nyumba wa 711 katika eneo la Kawe, unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), ulizinduliwa mwaka 2014 kwa gharama ya Shilingi Bilioni 105.11. Hata hivyo, mradi huo ulisitishwa mwaka 2018 baada ya kufikia asilimia 25 ya utekelezaji, kutokana na ucheleweshaji wa malipo kwa mkandarasi.

Mnamo mwaka 2022, baada ya NHC kulipa baadhi ya madeni ya awali, mkandarasi aliwasilisha madai ya nyongeza ya Shilingi Bilioni 49.09. Madai hayo yalihusisha gharama za ucheleweshaji, mabadiliko ya kazi, na athari za mfumuko wa bei. Bodi ya Wakurugenzi ya NHC yaliidhinisha madai hayo mnamo Desemba 2023 na hivyo kuongeza gharama ya mradi kwa asilimia 47.

SURA YA SABA



# Ukaguzi wa Hesabu za Miradi ya Maendeleo

## 7.1 Gharama za riba zinazoathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo - Shilingi Bilioni 71.47

Serikali inadaiwa Shilingi Bilioni 71.47 kama gharama za riba katika mwaka wa fedha 2023/24 kutokana na ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi, ukosefu wa fedha kwa wakati na changamoto za bajeti, ambapo kati ya deni hilo TANROADS inadaiwa Shilingi Bilioni 44.38 (asilimia 62 ya kiasi chote cha riba) inayotokana na mikataba mbalimbali na wakandarasi, Wizara ya Ujenzi Shilingi Bilioni 16.81 (asilimia 23 ya riba) ikiwa ni sehemu ya gharama za Daraja la Kigamboni chini ya NSSF. Hii inapelekea kupunguza uwezo wa kutekeleza mipango mipya ya maendeleo.



**Jedwali Na. 6: Taasisi zinazodaiwa riba**

| Taasisi | Riba (Shilingi Bilioni) | Asilimia |
|---|---|---|
| Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | 44.38 | 62.10 |
| Wizara ya Ujenzi | 16.81 | 23.52 |
| Kampuni ya Meli Tanzania (Marine Services Co. Ltd.) | 5.83 | 8.16 |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar Es Salaam | 3.16 | 4.42 |
| Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini | 0.71 | 0.99 |
| Wizara ya Maji | 0.27 | 0.38 |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza | 0.21 | 0.29 |
| Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro | 0.07 | 0.10 |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma | 0.03 | 0.04 |
| **Jumla** | **71.47** | **100.00** |

## 7.2 Ongezeko la Gharama Shilingi Bilioni 36.12 katika Utekelezaji wa Miradi

Tathmini ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo imebaini ongezeko la gharama zinazofikia jumla ya Shilingi Bilioni 36.12. Ongezeko hili limetokana na ucheleweshaji wa miradi, kasoro katika usanifu wa awali, malipo ya ziada kwa wakandarasi, pamoja na malipo ya fidia yasiyo na msingi wa kimkataba. Ongezeko la gharama za miradi linaongeza mzigo wa kifedha kwa Serikali na kuchelewesha utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo.

Mchanganuo wa gharama hizo unaonesha kuwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) anahusika na Shilingi Bilioni 18.88, sawa na asilimia 52 ya ongezeko lote, wakati Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) anahusika na Shilingi Bilioni 7.64, sawa na asilimia 21.1.




**Jedwali Na. 7: Taasisi zenye gharama za ziada**

| Taasisi | Taasisi Iliyo Husika | Gharama ya Ziada (Shilingi Bilioni) |
|---|---|---|
| TANROADS | Malipo ya ziada kwa wakandarasi kutokana na mabadiliko ya bei, ukiukwaji wa masharti ya mkataba wa mkopo na upembuzi yakinifu usio na uhalisia. | 18.88 |
| RUWASA | Malipo ya ziada yalitokana na uchunguzi duni wa wakandarasi, kusitisha mikataba kwa makubaliano na makosa ya usanifu. | 7.64 |
| DAWASA | Malipo ya ziada kufuatia tathmini mpya ya madai ya wananchi waliopitiwa na mradi wa Bwawa la Kidunda | 5.24 |
| H/Jiji Mwanza | Ukosefu wa tathmini ya miundombinu na makosa ya usanifu yalisababisha ongezeko la gharama. | 2.13 |
| DUWASA | Ongezeko la gharama kutokana na makosa katika usanifu. | 1.66 |
| H/Jiji Dar Es Salaam | Ukosefu wa tathmini ya hali ya miundombinu kabla ya ukarabati. | 0.57 |
| **Jumla** | | **36.12** |

## 7.3 Miradi inayotekelezwa kwa Kasi ndogo - Shilingi Trilioni 1.34

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya miradi 136 ya maendeleo yenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.34 inatekelezwa kwa kasi ndogo, kinyume na makubaliano ya kimkataba. Miradi hii imecheleweshwa kwa viwango vinavyotofautiana kati ya asilimia 1 hadi 92.

Miradi ya barabara chini ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) imecheleweshwa kwa kati ya asilimia 15 hadi 58, miradi ya maji inayosimamiwa na Wizara ya Maji na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa kati ya asilimia 1 hadi 83 na miradi ya afya na sekta nyingine imecheleweshwa kwa kati ya asilimia 32 hadi 92.

Sababu kuu ni usimamizi dhaifu wa mikataba, uwezo mdogo wa wakandarasi na ucheleweshaji wa fedha na utekelezaji. Hali hii imeongeza gharama, kuhatarisha manufaa yaliyokusudiwa na kuathiri ubora wa miradi.

## 7.4 Ufungaji wa Transifoma Zenye Uwezo Mdogo Kuliko Mahitaji ya Mradi

REA ilibadilisha aina za transifoma kutoka kVA 315 zilizopendekezwa kwenye upembuzi yakinifu na kuweka zenye uwezo mdogo (kVA 50, 100 na 200) bila kufanya uchambuzi wa mahitaji halisi ya umeme.

Mfano, katika mikoa ya Tabora na Mbeya, matumizi ya transifoma ndogo badala ya kVA 315 yameongeza hatari ya umeme kukatika mara kwa mara na kudhoofisha shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo.

## 7.5 Ucheleweshaji wa Matumizi ya Fedha za Maafa kwa Ajili ya Ukarabati wa Miundombinu Mkoani Manyara Shilingi Bilioni 7.01

Serikali ilitoa Shilingi Bilioni 11.13 kwa TARURA, BAWASA, TANESCO, na RUWASA ili kurejesha miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko mkoani Manyara (Desemba 2023). Hata hivyo, hadi Oktoba 2024 ni Shilingi Bilioni 4.12 (asilimia 37) pekee zilizotumika, huku Shilingi Bilioni 7.01 zikiwa hazijatumika kutokana na ucheleweshaji wa taratibu za manunuzi na utekelezaji duni wa miradi.

Pia, kukosekana kwa taarifa rasmi za utekelezaji kumeathiri uwajibikaji na uwazi na kuchelewesha urejeshaji wa huduma muhimu kwa wananchi.

SURA YA NANE



# Ukaguzi wa Ufanisi

## A. UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU USIMAMIZI WA HUDUMA ZA VIVUKO

### 8.1 Idadi Isiyojitosheleza ya Vivuko vilivyoko kwenye shughuli za Uendeshaji

Katika Ukaguzi huu, nimebaini kuwa kulikuwa na vivuko vilivyosimama kutoa huduma kutokana na kuongezeka kwa vivuko vilivyoharibika. Nimebaini kuwa, vivuko 11 kati ya 32 nchini havifanyi kazi, ambavyo ni sawa na asilimia 34 ya vivuko vilivyopo.

Pia, kulikuwa na huduma duni za vivuko kutokana na kutokuwepo kwa kivuko katika njia mpya zilizotambuliwa na kuharibika mara kwa mara, jambo lililosababishwa na utekelezaji usioridhisha wa matengenezo. Kutokana na hali hii, TEMESA ilikodisha huduma za kivuko kutoka kampuni binafsi ya usafirishaji majini ya Azam Marine na maamuzi haya yalichangia upotevu wa mapato.




## B. UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU UDHIBITI WA VYOMBO VYA USAFIRI MAJINI

### 8.2 Udhibiti Usioridhisha wa Vyombo Vya Usafiri Majini Vinavyomilikiwa na Serikali

Nimebaini kuwa vivuko 32 vinavyomilikiwa na TEMESA havikukidhi matakwa ya kiusalama majini. Vivuko hivi havikuwa na vyeti vya usalama majini, baadhi ya vivuko havikusajiliwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania. Kutokuwa na vyeti vya usalama majini kunamaanisha kuwa vyombo hivyo havikukidhi vigezo vya kiusalama vinavyotakiwa kwa vyombo vya majini ili viweze kusafiri bila tatizo.

Pia, Ukaguzi ulibaini kuwa vivuko vyote 32 vya TEMESA havikuwa na bima kinyume na Kanuni namba 4 ya Kanuni za Usafirishaji Majini za Mwaka 2011 ambazo zinataka vyombo vya usafiri majini kuwa na bima dhidi ya majanga yanayoweza kutokea. Kutokana na mapungufu hayo, Shirika la Uwakala wa Meli lilipaswa kuzuia vivuko hivyo kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Usafirishaji Majini ya Mwaka 2003 lakini halikufanya

hivyo. Kuendelea kufanya kazi kwa vivuko visivyokidhi vigezo vya kiusalama kunahatarisha usalama wa watumiaji na vyombo vyenyewe.

## C. UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU USIMAMIZI WA MAFURIKO

### 8.3 Upangaji na Uandaaji wa Bajeti Usio Tosheleza katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya Shughuli za Maandalizi ya kuzuia Mafuriko na majanga Katika Maeneo Yao

Katika ukaguzi huu, nimebaini kuwa Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa hazikutenga bajeti ipasavyo kwa ajili ya maandalizi ya kukabiliana na mafuriko na majanga mengine ya dharura. Kati ya halmashauri sita zilizokaguliwa, ni Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji pekee ndiyo iliyotenga bajeti kwa madhumuni haya. Halmashauri hiyo ilitenga Shilingi milioni 60 kwa mwaka wa fedha 2022/23 na Shilingi milioni 10 kwa mwaka wa fedha 2023/24. Halmashauri nyingine tano hazikutenga bajeti yoyote kwa ajili ya maandalizi ya kukabiliana na majanga katika kipindi cha miaka ya fedha 2020/21 hadi 2023/24.

Ukosefu wa vifungu maalum vya bajeti na maelekezo kutoka Wizara ya Fedha uliathiri uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga fedha kwa ajili ya maandalizi dhidi ya mafuriko, na kudhibiti majanga. Matokeo yake ni kuongezeka madhara kama vifo, uharibifu wa mali, mazao, barabara, na majengo kipindi cha mafuriko nchini.

## D. UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU USIMAMIZI WA HALI YA HEWA

### 8.4 Vituo Binafsi vya Hali ya Hewa Vilifanya Kazi Bila Vibali kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa

Katika Ukaguzi huu nimebaini kuwa vituo vingi binafsi vya hali ya hewa vilifanya kazi bila vibali kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa, kinyume na Kifungu cha 19(1) cha Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa ya mwaka 2019. Takwimu zinaonesha kuwa kati ya mwaka wa fedha 2019/20 na 2023/24, idadi kubwa ya vituo binafsi vya hali ya hewa havikuwa na vibali, huku asilimia 100 ya vituo vikifanya kazi bila vibali mwaka 2019/20, na idadi hiyo ikishuka hadi asilimia 96 mwaka 2022/23.

Hali hii ilisababisha Mamlaka ya Hali ya Hewa kushindwa kukusanya shilingi milioni 303.09 kutokana na ada za vibali vya hali ya hewa pamoja na kiasi cha cha shilingi milioni 105.9 kutokana na ada za usajili wa vituo vya huduma za hali ya hewa nchini. Ukosefu wa vibali umesababisha upotevu wa mapato kwa Mamlaka ya Hali ya Hewa na kudhoofisha usimamizi wa taarifa za hali ya hewa, hali inayoweza kuathiri sekta kama kilimo, usafirishaji na usimamizi wa maafa.

## E. UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU UDHIBITI WA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA

### 8.5 Ufuatiliaji Hafifu wa Ubora wa Dawa za Tiba Asili

Katika Ukaguzi huu nimebaini kuwa Baraza la Tiba Asili na Mbadala (TAHPC) halina mfumo endelevu wa ufuatiliaji wa ubora wa dawa za tiba asili. Tangu mwaka 2021 hadi 2023, Ukaguzi wa dawa kwenye soko umefanyika mara mbili pekee, ikiwa mbali na mapendekezo ya mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) unaosisitiza usimamizi wa mara kwa mara wa

dawa za tiba asili. Kukosekana kwa ufuatiliaji thabiti kumesababisha dawa za tiba asili kuuzwa bila kufanyiwa upimaji wa ubora na usajili rasmi, hali inayoongeza hatari kwa afya ya Umma. Waganga wengi hawajasajili dawa zao kutokana na gharama kubwa za usajili na ukosefu wa uelewa kuhusu mchakato wa kuthibitisha ubora wa dawa zao. Ukaguzi pia ulibaini kuwa baadhi ya dawa zinauzwa bila kufuata viwango vilivyowekwa na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, hali inayosababisha athari kwa wagonjwa wanaotumia tiba hizi.

## F. UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU UFANISI WA GHARAMA KWENYE MIFUMO YA TEHAMA ILIYOUNDWA NA WATAALAM WA NDANI WA TAASISI ZA UMMA

### 8.6 Utekelezaji Usio jitosheleza wa Hatua za Kudhibiti Gharama katika Mipango na Upataji wa Mifumo ya TEHAMA

Katika Ukaguzi huu, nilibaini kutoshirikishwa kikamilifu kwa wadau, hasa katika mifumo ya TEHAMA sita kati ya 12 iliyokaguliwa ambapo wadau wa ndani walihusishwa kwa kiwango kidogo zaidi. Aidha, mifumo 11 kati ya 12 ya TEHAMA ilihusisha wadau wa nje kwa kiwango kidogo kuliko ilivyohitajika.

Hali hii ilisababishwa na uratibu usiojitosheleza wa kuwahusisha wadau wakati wa kutathmini miradi na hivyo kusababisha uwezekano wa kuwepo kwa vihatarishi na mifumo iliyozinduliwa kuwa na vipengele vinavyoshindwa kufanya kazi kwa ufanisi unaotarajiwa.

## G. UKAGUZI WA UFANISI UNAOHUSU UTOAJI WA HUDUMA ZA UGANI WA MIFUGO

### 8.7 Upungufu wa Rasilimali Watu, Fedha na Vifaa vya Kufanyia Kazi za Huduma za Ugani za Mifugo

Katika Ukaguzi huu nilibaini kuwa kulikuwa na upungufu wa maafisa ugani nchini. Kulikuwa na maofisa ugani 4,406 tu (sawa na asilimia 33) kati ya maofisa Ugani 13,279 waliohitajika. Tathmini ya Kitaifa ya mwaka 2024, ilibainisha kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilifanikiwa kusambaza pikipiki 1,500 kati ya 4,406 zilizodaiwa kuwezesha kuhudumia Maafisa Ugani wa Mifugo kote nchini. Usambazaji wa pikipiki ulifikia asilimia 34 tu ya mahitaji yaliyopo. Upungufu wa rasilimali watu, fedha na vitendea kazi ilipelekea asilimia 9 tu ya kaya 2,747,910 za wafugaji kupatiwa huduma za ugani wa mifugo nchini.



SURA YA TISA



# Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA

## A. MFUMO WA UHASIBU WA MUSE

### 9.1 Mapungufu katika Mgao wa Fedha kutoka Hazina (Exchequer)

Mfumo uliruhusu mgao wa fedha kwenda kwenye vifungu vya malipo kuzidi jumla ya kiasi kilichopokelewa na Taasisi kutoka Hazina. Hii inasababisha hatari ya matumizi kuzidi bajeti iliyoidhinishwa.

### 9.2 Udhibiti Hafifu wa Malipo ya Masurufu (Imprest)

Mfumo wa MUSE unaruhusu vocha za malipo ya masurufu (Imprest) zaidi ya moja kwa ombi hilohilo moja, hali inayosababisha kufanyika kwa malipo mara mbili (Double payment).

### 9.3 Mapungufu katika Usimamizi wa Mapato

Mfumo wa MUSE ulishindwa kutofautisha mapato ya mwaka huu na madeni ya miaka iliyopita yanayokusanywa kupitia GePG, hali iliyosababisha mapato yote kuoneshwa kama yamekusanywa ndani ya mwaka huu. Kutokana na hilo, taarifa za mapato na madeni zilipotoshwa.

## 9.4 Matumizi ya Mifumo ya Uhasibu miwili

Chuo cha Mzumbe, TBS na Bodi ya Pamba vilitumia mifumo miwili tofauti ya uhasibu kutokana na mfumo wa MUSE kushindwa kutunza taarifa za madeni, hali inayosababisha kupoteza ufanisi na kuongeza gharama za usimamizi wa mifumo.




## B. MIFUMO YA MAPATO

## 9.5 Matumizi ya API kwa Ufuatiliaji wa Uhamisho wa Mapato

Kutotumiwa kwa ukamilifu API iliyoundwa na Wizara ya Fedha kufuatilia uhamisho kamili na ule wa kuchelewa wa mapato kutoka Akaunti za Makusanyo za Benki za biashara kwenda Benki ya Tanzania. Ninapendekeza kutumika kwa API hiyo kikamilifu hasa katika kutambua kwa wakati ucheleweshaji wa uhamisho wa makusanyo kwenda Benki ya Tanzania.

### 9.6 Tofauti Kati ya Mifumo ya Ukusanyaji Mapato na GePG Kutokana na Kushindwa Kupokea Taarifa kutoka Benki

Ukaguzi ulibaini kuwa malipo yaliyorekodiwa katika mifumo ya MU-ARMS, Car Parking Management System na NAVS katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, TAA, na NACTVET hayakuonekana kwenye GePG kwa sababu benki za kibiashara hazikutoa taarifa kwa GePG baada ya malipo kufanyika. Hali hii ilisababisha mapato katika GePG kuonekana pungufu na kuathiri usahihi wa taarifa za ukusanyaji mapato.

### 9.7 Mapungufu ya Mfumo wa MAJI-IS yaliyopelekea Kutokutozwa Ada za Matumizi ya Maji na Huduma za Maji Taka kwa Wateja Hai

Wateja waliosajiliwa walitumia maji bila kutozwa ada kutokana na hali ya mita zao kuwa "hazijulikani" katika mfumo ingawa zilikuwa zinajulikana na kutumia maji. Pia, Ukaguzi ulibaini kuwa wateja wanaotumia huduma za maji taka hawakutozwa ada za maji taka kutokana na hitilafu za usanidi wa mfumo.

## C. MATUMIZI YA MIFUMO YA TEHAMA

### 9.8 Kutotumika kwa Mifumo kwa Ufanisi

Taasisi kadhaa kama TAA, CRB, UDOM, TEMESA, TANAPA, GPSA, NIC, TANROADS na DAWASA hazijatumia ipasavyo mifumo yao ya TEHAMA. Moduli kama za usimamizi wa hesabu ya mali, usimamizi wa magari, ufuatiliaji wa mapato, manunuzi na malipo vimebaki bila kutumika, hivyo kupunguza ufanisi wa kiutendaji na kurudisha nyuma thamani ya uwekezaji katika mifumo hii.

## 9.9 Matumizi ya mifumo miwili yenye majukumu sawa kwa wakati mmoja

Manispaa ya Ubungo, TAMISEMI, TANGAUWASA, ATCL, TANESCO na TRA walikuwa wakitumia mifumo miwili kwa kazi zinazofanana. Hii ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Serikali mtandao, inayotaka kuondoa mifumo inayofanana kupunguza gharama za usimamizi wa mifumo.

## D. MKAKATI WA KITAIFA WA USALAMA WA MTANDAO

## 9.10 Kukosekana kwa Kituo cha Kitaifa cha Usimamizi wa Usalama wa Mtandao (NSOC)

Kituo cha NSOC kilichopangwa kuanzishwa hakijaanzishwa na TZ-CERT, kinachofanya kazi chini ya TCRA, hakijakidhi mahitaji ya kusimamia masuala yote ya usalama wa mtandao kwa kiwango cha Kitaifa. Hali hii imeacha ombwe katika usimamizi wa matukio ya kiusalama wa mtandao.

## 9.11 Kushindwa Kutambua na Kusajili Miundombinu Muhimu ya TEHAMA ya Kitaifa (NCII)

Hakuna rejista ya miundombinu na mifumo muhimu ya kidijitali hali inayoiweka nchi katika hatari ya mashambulizi ya mtandao kwa kuwa miundombinu na mifumo hii muhimu ya kidijitali haipewi kipaumbele ili kuweza kulindwa ipasavyo.

## TOLEO MAALUM LA MWANANCHI




**Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**
**4 Barabara ya Mahakama**
**S.L.P 950, Tambukareli, 41104 Dodoma**
**Simu: +255 (026) 2161200**
**Barua Pepe: ocag@nao.go.tz**

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT
ISO 9001:2015 Certified